



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI
(RITA)



NOTISI KWA WADHAMINI WA TAASISI/ASASI NCHINI

Kabidhi Wasii Mkuu ambaye ndiye Msimamizi Mkuu wa Wadhamini, anawatangazia wadhamini wa taasisi na asasi zote nchini zilizosajiliwa RITA kufanya Marejesho kila mwaka kwa wakati pamoja na kuwasilisha taarifa kama kuna mabadiliko ya wadhamini, anuani, katiba, jina la Taasisi/ Asasi na ofisi kwa mujibu wa Sheria ya Usajili wa Wadhamini, Sura ya 318 Toleo la 2002.

Notisi ya siku 30 inatolewa kuanzia leo **ijumaa, Tarehe 29 Mei, 2020** ili kutoa nafasi ya kutekeleza maelekezo haya na watakaoshindwa watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria ikiwemo kufutwa kwa Taasisi /Asasi wanazozisimamia.

Marejesho yanaweza kuwasilishwa/kutumwa kwa njia zifuatazo:

Ofisi za RITA Makao Makuu, Ghorofa ya Nne- Jengo la RITA, Mtaa wa Simu na Makunganya, Dar es Salaam

Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu,
S.L.P. 9183,
4 Mtaa wa Makunganya
11104 Dar es Salaam.

Kwa barua pepe : info@rita.go.tz.

Kwa maelezo zaidi piga simu(Bila malipo) namba **0800 117 482** au tembelea
Tovuti ya Wakala **www.rita.go.tz**

Emmy K. Hudson
Kaimu Kabidhi Wasii/ Afisa Mtendaji Mkuu
28 Mei, 2020